East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 4, Issue 1, 2019
ISSN: 1476-4687

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# VIPENGELE VYA MWINGILIANOMATINI KATIKA UJENZI WA MAUDHUI YA UMASKINI: MFANO KATIKA MUSALEO! NA BINA-ADAMU!

*Esther J.Korir[1], Prof. Issa Mwamzandi[2] & Dkt. Simiyu Kisurulia[3]*

[1]Chuo Kikuu cha Kabianga, SLP 2030 – 20200, Kericho, Kenya, estherkorir44@gmail.com.
[2]Chuo Kikuu cha Kabianga, SLP 2030 – 20200, Kericho, Kenya, imwamzandi@yahoo.com.
[3]Chuo Kikuu cha Kabianga, SLP 2030 – 20200, Kericho, Kenya, kisurulia@gmail.com.

**Article history:**

*Received: 13 Oct 2019*
*Accepted: 16 Oct 2019*
*Published: 24 Oct 2019*

**Keywords**:

*Mwingilianomatini, umasikini, Musaleo! Bina-Adamu!*

**IKISIRI**

Makala haya yanatathmini matumizi ya vipengele vya mwingilianomatini (MM) katika ujenzi na uwasilishaji wa maudhui ya kazi za Kiswahili. Uchanganuzi huu ni wa kimaktaba kufuatia mihimili ya nadharia ya Mwingilianomatini. Riwaya za *Musaleo!* na *Bina-Adamu* zilichaguliwa kimakusudi kwa sababu mwingilianomatini umetumiwa kujenga dhamira ya umaskini. Maudhui ya ulitima katika riwaya za *Musaleo!* na *Bina-Adamu* yamechaguliwa ili kudhihirisha jinsi suala sumbufu ulimwenguni linaweza kuwasilishwa kwa njia mbalimbali. Waandishi wa kisasa wa fasihi wamechangamkia mno matumizi ya mbinu ya mwingilianomatini katika ujenzi wa dhamira za kazi zao. Riwaya za *Musaleo!* na *Bina-Adamu* za Wamitila zilirejelewa kama mifano ya kazi zilizojengwa Ki-MM. Riwaya za kisasa ni muhimu katika jamii kwani maandishi yanahusu masuala yanayomkumba binadamu katika ulimwengu wake sasa, anapojaribu kujitambua na kujieleza.

## UTANGULIZI

Mwingilianomatini ni dhana inayohusishwa na mwananadharia wa Kifaransa, Julia Kristeva. Kristeva ni Mwanafalsafa wa asili ya Kibulgaria na Ufaransa aliyezaliwa mwaka wa 1947. Aliasisi nadharia ya Mwingilianomatini, (MM)ilitokana na nadharia ya Bakhtin ya Usemezano mnamo mwaka wa 1966. Dhana hii hutumiwa kuelezea kuwepo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya kifasihi.

Kristeva ni miongoni mwa wananadharia wa Baadausasa, wakiwemo Barthes, Derrida, Foucault, Lacan na Althusser. Katika kazi zake za "*The Bounde Text"* na *"Word Dialogue and Novel*", Kristeva, anachota kutoka kwa kazi za Mikhail Bakhtin na Umuundo wa Kirusi, ili kuasisi dhana ya MM ambayo baadaye ilihusishwa na maendeleo katika Baadaumuundo (Selden,Widdowson & Brooker, 2005).

Katika fasihi kuna usemezano baina ya kazi kadhaa kati ya mwandishi na mwandikiwa, na miktadha ya tamaduni za sanaa za awali (Kristeva, 1980). Kulingana na Kristeva, MM huchunguza chanzo halisi cha matini na mkusanyiko wake wa ujuzi wa kifasihi na kitamaduni ambao hujengwa kutokana na athari za matini nyingine. Wasomaji

huibua maana ya matini wanazozisoma na ikawa kama sehemu ya usemezano unaoendelea kati yao (na pia mwandishi) kulingana na muktadha, sehemu ya matini au matini nzima. Msomaji ana wajibu wa kutambua sehemu za MM katika matini inayosomwa kulingana na tajiriba yake ya kitamaduni, kiusomi na kielimu.

Mwingilianomatini hurejelea njia ambazo usemezano katika maandishi au matamshi hulenga maneno, mifumo ya kiisimu au ya kisarufi ya mzungumzaji wa awali ama mazungumzo fulani. MM huweza kutokea kimaksudi kama vile wakati mwandishi anaponukuu ama kutaja kazi ya msanii mwingine. Shughuli hii hutendeka mno hasa watu wanapozungumza (Tyson, 2006). Tyson anachukulia kwamba kila kazi ya kifasihi inahusiana na kazi iliyoandikwa awali kwa namna moja au nyingine. MM hupata maana kupitia kwa msaada wa kazi nyinginezo. Mwandishi hapa hukopa matini na nukuu ili kusisitiza maana ya kazi yake.

Olali (2010), anafafanua hali ya kuwepo kwa riwaya za kimajaribio na riwaya kadha za Kiswahili zilizoandikwa tangu miaka ya 1990 hadi leo. Riwaya hizi zinazodhihirisha miundo isiyo ya kawaida zikilinganishwa na miundo ya riwaya za kihalisia. Riwaya mpya hutumiwa kueleza aina ya riwaya ambayo inakiuka sheria za kawaida za utungaji na muundo wa riwaya, (Wamitila, 2003). Mtindo huu wa utunzi umewezesha hali ya kukabiliana na mabadiliko kadha yanayo zikumba jamii zetu za kisasa. Bila kuwepo kwa nafasi hii, waandishi wengine wangepata ugumu katika kueleza mabadiliko hayo. Riwaya hizi huitwa "riwaya za kimajaribio," dhana inayotumiwa kurejelea riwaya zilizozuka Ufaransa katika miaka ya 1950 na kuakisi matumizi ya mbinu za kiubunifu za uandishi wa riwaya. Mifano ya Riwaya hizi mpya za Kiswahili ni kama vile *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za E. Kezilahabi, *Bina-Adamu! (*2002) na *Musaleo! (*2004) za Wamitila, *Babu alipofufuka* (2002) na *Dunia yao* (2006) za S. A. Mohamed, *Mafamba* (2008) na *Watu wa Gehena* (2012) za Tom Olali miongoni mwa riwaya nyingine.

*Bina-Adamu*! na *Musaleo!* ni riwaya zinazosemekana kuwa riwaya za kisasa ambazo miongoni mwa sifa nyinginezo, zimefafanuliwa kama zinazotumia MM kama mbinu kuu ya kiuandishi. Riwaya hizi za kisasa zimeandikwa kwa ustadi wa kimwingilianomatini (Ki-MM) na huwa tata mno kueleweka miongoni mwa wasomaji.

Hebel (1989) na Simmons (2013) wanakubaliana kuwa kuna aina tatu za MM. Aina ya kwanza ni ile ya lazima; ambapo mwandishi hutumia mlinganisho wa moja kwa moja kati ya matini mbili tofauti. Hapa kwa mfano mwandishi huchagua kutaja mambo hadithini ambayo msomaji tayari huwa anaelewa chanzo kwa vile amewahi kukumbana nayo katika matini za awali. Aina ya pili ni ile ya hiari; aina hii hurejelea matini za awali pekee na si lazima msomaji awe amezipitia ili aweze kuelewa matini inayosomwa au matendo ya mhusika anayerejelewa. Aina ya tatu ni marejeleo yanayofanywa bila kukusudia. Katika hali hii hupatikana uhusiano kati ya matini, desturi, mila na tajiriba za msomaji ambazo zinajitokeza kutoka kwenye matini anayoisoma. Hali hii inategemea tanzu kama vile methali, ngano au hadithi za bibilia azijuazo msomaji.

Katika nadharia hii ni bayana kuwa matini husheheni mpangilio wa matini zilizobadilishwa, na ambayo huwa na matamshi kutoka kwa matini nyingine ambazo huoana na kukamilishana. Utafiti huu uliangalia msingi mpana wa Ki-MM kama ulivyoelezwa na Kristeva. Mawazo yake ni kuwa fasihi hutokana na kuwepo kwa fasihi nyingine ulimwenguni. Mambo muhimu yanapaswa kuchunguzwa katika matini kwa kutegemea nadharia ya MM kulingana na Kristeva na kufafanuliwa na Wamitila (2008).

Uhusiano kati ya matini au kazi moja na nyingine huweza kuathiri au kuwa na mchango kwa maana na dhamira ya kazi zinazohusika. Mchanganuzi anapaswa kuchunguza mahusiano yenyewe na kuonyesha ni kwa namna gani ambavyo mahusiano hayo yanaathiri sifa tofauti za kazi inayorejelewa. MM haiathiri tu dhamira na maudhui bali huweza pia kuingiza sifa za ki-itikadi. Riwaya hizi za kimajaribio zinatumia ukumbukaji na urejelezi mwingi na tamaduni zinaingiliana mbali na mandhari na nyakati. Aina hizi tatu za MM hutumika kutegemea malengo ya mwandishi ya kutaka tu kurejelea ama kuendeleza maudhui anayo yashughulikia. *Musaleo!* na *Bina-Adamu* ni riwaya zilizobainisha matumizi ya MM na vipengele

vingine changamano ili kufaulisha ujumbe na ukamilifu wa hadithi zilizowasilishwa. Riwaya hizi mbili zinaponukuu maandishi na kurejelea visa, hadithi na matukio mengi kutoka kwa mazingira tofauti tofauti ulimwenguni, vipengele hivyo vyote vita angaziwa.

## UMASKINI

Umaskini ni hali ya ukosefu wa mahitaji ya kimsingi ya kibinadamu kama vile chakula, maji, usalama, mavazi, nyumba na huduma za afya kutokana na uwezo wa kuvinunua (TUKI, 2004).Ulitima ni udhaifu wa maisha unaotokana na shida kuu za kiuchumi, na huweza kusababishwa na mfumo mbaya wa utawala wa kikoloni na ukoloni mamboleo. Mwandishi anaelezea hali hii ya ulitima kwa kurejelea hali mbali mbali zinazodhihirika katika jamii. Anafanya hivi Ki-MM kwa kutumia nukuu, istilahi na hata marejeleo ya kazi za awali na misimu inayotumika katika jamii.

Maudhui ya ulitima yamejengwa kwa njia mbalimbali ikiwemo MM ili kuonyesha katika hadithi hizi hali ilivyokuwa awali na sasa barani Afrika. Mbinu hii ya MM imeonyesha namna ambavyo hali ya ulitima ulivyo lemaza Afrika hadi sasa. Mwandishi anarejelea hali za kihistoria na pia kutabiri hali itakavyo kuwa siku za usoni. Hali mbaya ya uongozi ulioletwa na mkoloni unafanya hali ya umaskini kukita mizizi. Isitoshe, viongozi wabadhirifu na wasiowajibika wameendelea kudidimiza Waafrika katika lindi la ulitima. Kupitia MM mwandishi anauliza, umio hili la umaskini ulisababishwa na nani au nini? Baada ya kupata uhuru viongozi wamefanya nini ili kuokoa raia kutokana na hali hii? Kwa nini hali hii inaonekana kuimarika katika nchi nyingi barani?

## VIPENGELE VYA MM VINAVYOJENGA UMASKINI KATIKA *MUSALEO!*

Hadithi ya *Musaleo!* inapoanza, mwandishi anavuta taswira ya msomaji kwa watoto wanaovuta bangi chini ya mti. Hali ya umaskini imebadilisha amali zilizoenziwa tangu jadi katika jamii za Kiafrika. Hali hii inafafanuliwa wazi na mwandishi anaporejelea hali nyingine duni za jamii ambazo ziko nje ya bara la Afrika. Msimulizi anasema:

Hawa wahuni wanawafunza wanetu kuvuta bangi...itabidi tujaribu kufanya jambo. Wanafurika mjini hawa....”(uk 1).

Nukuu ya maneno ya mkaazi wa kijiji inatolewa moja kwa moja na kujenga maudhui ya umaskini. Mfumo wa uongozi ulipobadilika kutoka ule wa ukoloni mkongwe hadi ukoloni mamboleo, utamaduni wa Waafrika uliathirika na uchumi wao kutatizika. Umaskini wa mali na ule wa maadili ulibainika. Hali ya maisha ilipobadilika kutoka kwa ile ya ufugaji, uwindaji na kuhamahama, Waafrika walilazimika kwenda kuwatumikia Wazungu na watoto wakabaki chini ya ulinzi wa vijana wenzao. Uigaji wa mienendo mbovu ukasababisha hali hii ya kuvuta bangi.

Vijana wasio na kazi wamezidi kuongezeka katika jamii na mwandishi anafananisha hali hii na ile ya mji wa “*Rio de Jenairo* nchini *Brazil*” (uk 25). Kwa kutaja *Rio de Jenairo* Ki-MM, mwandishi amepanua kumbukizi za msomaji kwa kulinganisha hali duni ya vijana wanaokosa kazi nchini na hali ilivyo katika mji wa Rio de Jenairo. Wao wanazurura mijini na msimulizi anasema kuwa wakati mwingi vijana hawa huvamiwa kwa sababu ya kutuhumiwa kwa wizi na maovu mengine. Hali yao ya ukata unaashiria kuwa jamii za ughaibuni na hizi za Kiafrika zimekosa kuwaadhibiti vijana wake.

Hali ya umaskini katika jamii za Kiafrika ilisababishwa na mfumo ulioanzishwa na mkoloni wa kuchukua sehemu za ardhi zenye rotuba na kumwachia Mwafrika sehemu ngumu au ‘Mashamba ya Mawe...’. Msimulizi anasema:

“Ukolongwe alitumia ujanja wake. Ardhi yote iliyokuwa na rutuba aliichukua na kuwakabidhi jamaa zake hao”(uk 27).

Wakoloni hawa waliendelea kujiimarisha kiuchumi huku Waafrika wakifanywa kuwatumikia katika mashamba yao makubwa. Umaskini uliendelea kuwauma Waafrika kwa sababu hawakuwa na nafasi ya kufanya kazi katika mashamba yao binafsi, mbali na kwamba yalikuwa ya mawe.

Mwandishi anaangazia suala la umaskini uliowakumba wale waliofanya juhudi kuhakikisha kuwa nchi yao imepata ukombozi kutoka kwa minyororo ya ukoloni. Hawa wapiganaji wa uhuru

waitwa “War Veterans*”* ambao wanadaiwa kuwa waliifanyia nchi yao kazi kubwa lakini *‘waliishi katika vibanda dhaifu na waliochongwa na ala za maisha ya dhiki’* (uk 14).

Mwandishi anataka kusisitiza hapa kuwa hali ya ukata haikusababishwa na ukoloni pekee bali pia tamaa na ubinafsi wa viongozi wa asili ya Kiafrika walioshika hatamu za uongozi baada ya kuondoka kwa mkoloni. Baada ya uhuru katika nchi hizi za Kiafrika, hali haikubadilika sana kwa vile Waafrika wengi hawakumiliki mali. Umaskini unadhihirika kule Balawa alipozuru Msimulizi na kushuhudia kijana mchuuzi akinusurika kugongwa na gari. Biashara yake ndogo ilikuwa karibu kuangamia na anamweleza msimulizi kuwa: “Tunauza tu kujitafutia chakula. Kwa nini hatutakiwi jijini? Tume wakosea nini wenye magari?” (uk 28).

Msimulizi anapoelekea mkabala wa jengo la Balawa alimpata kipofu aliyeegemea ukuta akiwa na kikebe chake cha kuombea mapeni. Mwandishi anafafanua uozo kwa kunukuu moja kwa moja maneno yake aliposema; *“Sasa watamnyang’anya pesa zake yule kipofu” (uk 32).* Umaskini unawasukuma vijana wanaozurura kuiba kutoka kwa watu bila hata kuwaonea huruma mnyonge mwenzao. Hata yule kijana aliyekuwa akitafutwa na Msimulizi, alionyesha dalili zote za ulitima kwani tunaelezwa Ki-MM kuwa:

“Mararu yake yalikuwa yamechukua rangi ya bereu kama kwamba alichezea mafuta ya gari. ‘Hawa watoto wanavuta na kunusa gundi, wanaishi katika ulimwengu tofauti,’ nili ikumbuka sauti ya jirani yangu aliyelalamika kuwahusu” (uk 32).

Mwandishi anawaangazia vijana hawa kwa nia ya kuitanabahisha jamii kuwa sera ya ugavi wa rasilmali za jamii inafaa iangaliwe upya na viongozi wa mataifa ya Kiafrika. Vijana ni nguzo ya jamii na iwapo mabadiliko hayatafanywa, hali hii ya umaskini itaendelea kushuhudiwa kwa kiwango kikubwa. Wakati wa mapinduzi walikataa kabisa kwenda shuleni na hali hii ikazidisha ulitima katika jamii (uk 76). Mwandishi ametumia mbinu ya kunukuu moja kwa moja ili kuyajenga maudhui ya umaskini ulioshuhudiwa. Matumizi ya dawa za kulevya na kutopata elimu bora hufanya jamii yoyote ile kuselelea katika hali ya maskini kwa muda mrefu.

Kwingineko katika hadithi, mwandishi anatumia mbinu ya kurejelea istilahi maalum ya msimu Ki-MM ili aweze kujenga hali ya umaskini. Nesi aliyekuwa akifanya kazi na Dr. Mm’ati Mort anadai kuwa mgonjwa hawezi kutibiwa kwa sababu Hospitali haina vifaa vya upasuaji na daktari naye ameenda likizoni mbali na kukosa ‘gari la ambulansi’ (uk 72). Umaskini huu umekita na kuingia katika sekta mbalimbali za mataifa haya huru na hivyo kuwa suala linalohitaji kukabiliwa na viongozi wanaokuza sera muhimu. Utegemezi wa nchi za kigeni kupata misaada, uliwafanya Waafrika wengi kuwa maskini. Mataifa haya yanasubiri ufadhili wa kununulia dawa na vifaa muhimu vya utabibu badala ya kuvumbua vyao. Viongozi wa nchi hizi aidha, hawakubuni miundo na sera nzuri za kiuchumi kwa mataifa yao changa.

Katika maelezo ya mwandishi, ‘mitumba ya marehemu *George’* (uk 90) inazungumziwa Ki-MM. *‘George’* anayetajwa hapa pengine ni mzungu aliyekuwa wa kwanza kulitumia vazi linalorejelewa. Mwandishi anaikejeli hali hii duni ya Waafrika wanaodai kuwa huru ilhali bado wanategemea bidhaa duni kutoka ng’ambo ili kukidhi mahitaji yao ya kimsingi kama vile mavazi. Katika muktadha huu, wanafanya hivyo kwa kutegemea masalio ya Wazungu ambao ni marehemu. Wanastahili kuvumbua viwanda vyao na kutumia malighafi kutoka kwa nchi zao. ‘Marehemu *George’* ni msimu unaotumiwa katika muktadha wa mazungumzo ya vijana katika mazingira ya Kenya.

Katika kisa kingine, mwandishi anatumia mhusika tofauti na wengine. Mhusika kichaa anayerejelewa kuwa hali yake ilikuwa mbaya kufuatia hali ya ulitima, aliona kuwa ucheshi tu ndio ubobo katika mifupa ya uhai wao. Waliomsikiliza walidai kuwa lazima alimjua *‘Aristotle’* au lazima alisoma na *‘Europides’* (uk 91). Mwandishi anawarejelea hawa wawili Ki-MM kwani wasomaji hawajakutana nao hadithini. Hii ni ithibati kuwa hali mbaya ya ulitima imewaathiri Waafrika wengine kisaikolojia na si jambo jepesi.

*‘‘Aristotle na Europides’’* ni wanafalsafa wawili wa asili ya Kigiriki walioanzisha tanzia za kuliwaza jamii kabla ya kuzuka na kuwepo kwa futuhi. Waliamini kuwa uchungu ulifikia kiwango cha kuleta utakaso nafsi. Hali mbaya ya ulitima

ilimfanya mhusika kuwa wehu ili aweze kusahau makali yake ambayo hana uwezo wa kuyabadili. Mawazo haya yametumika Kimwingilianomatini na msomaji ambaye hajawahi kupitia matini hizo za Kigiriki ataweza kutatizika mno na kukosa hamu ya kuisoma riwaya hadi mwisho. Mwandishi hata hivyo ameweza kujenga maudhui yake kutalii hadithi na visa vya asili ya Kigiriki na kutumia kufafanua na kutilia mkazo shida zinazokumba jamii.

Hali ya umaskini imesababisha matatizo mengi kwa umma na suluhisho halipatikani kwa urahisi. Mwandishi anamtoa msomaji nje ya fasihi za Kiafrika na kurejelea matini ya Kigiriki ya "*Oedipus Complex"* (uk 90) ambapo '*Sphinx'* ni dude linalosumbua umma na viongozi wa nchi hiyo wanashindwa kupata suluhu la kudumu. Katika kisa hiki, Sphinx alikuwa dude sumbufu ambalo lilikuwa limehangaisha eneo la Thebes huko Ugiriki. Lilisababisha ukame na njaa na lilidai kuwa lingetoka katika eneo hilo tu iwapo wenyeji wangelijibu fumbo lake.

Fumbo lilikuwa ni kutambulisha kiumbe chenye miguu miwili, mitatu au minne na ambaye ingawa anaweza kubadilisha umbo lake, linatembea polepole mno linapotumia miguu mingi. Yeyote aliyeshindwa kufumbua fumbo hilo, angeuawa na kuliwa na Sphinx. Oedipus alijitolea kujibu fumbo baada ya mfalme wa Thebes kutoa zawadi ya kumtunuku himaya na bintiye kwa yeyote aliyefaulu. Oedipus alipotoa jibu sahihi Spinx alikasirika mno na akajirusha chini kutoka ulingo mrefu na akafa. Kupatikana kwa suluhu la tatizo hili la umaskini si jambo rahisi kama anavyorejelea mwandishi kupitia kwa kisa hiki cha Sphinx na Oedipus. Mwingilianomatini hapa, ni mbinu anayotumia mwandishi kuonyesha uhuru wa kurejelea matini zozote zinazoweza kujenga matini inayo shughulikiwa.

Matabaka mawili ya matajiri na maskini yamezungumziwa mno kwa sekta ya kiafya, makao na masomo. Umaskini ni hali ambayo imekumba nchi nyingi lakini tofauti na kijiji cha Mzee, wao wamebuni njia za kujimudu na kujiendeleza. Watoto wanaorandaranda mjini *Rio de Jenairo* ni wa hali moja na Ombaomba wa nchi hizi. Watoto wanapokosa malezi bora na makazi katika jamii yoyote, hii ni ishara kamili kuwa jamii hiyo ni maskini.

Umaskini ni hali inayotokana na mfumo mbaya wa utawala na mabadiliko muhimu yakifanywa suluhu linaweza kupatikana. Hii hali imeleta madhara mengi kwa waathiriwa na mwandishi ameweza kuiangazia kwa kunukuu mawazo au mazungumzo ya watu mbali mbali wa zamani au wa sasa. Istilahi zinazopatikana katika jamii pia zimetumiwa kuyajenga maudhui haya. Fasihi za maeneo tofauti na yale anayotoka mwandishi pia zimetumiwa kuyajenga maudhui haya. Vipengele vya MM vinavyojenga Umaskini Katika *Bina-Adamu!*

Mkoloni alipomtawala Mwafrika kisiasa, kiuchumi na kitamaduni, aliacha athari kubwa mno maishani mwake na Mwafrika hana budi kuzungumzia masuala hayo kwa karne nyingi. Katika riwaya ya *Bina-Adamu!*, wenyeji hawakusazwa na umio la umaskini. Mwandishi anafafanua hali hii ya ukata kuanzia wakati wa ukoloni mkongwe, ukoloni mamboleo na athari zake kwa maisha ya Waafrika kwa jumla. Mwandishi anajenga maudhui haya kwa kutumia nukuu za Bibilia, marejeleo ya kazi za awali, kutaja baadhi ya istilahi za jamii ya Kiafrika na hata kutumia vipengele vya fasihi simulizi.

Msimulizi anatufunulia hali ya umaskini unaoangaziwa katika kijiji chake cha Zakongwe inayosimamia bara la Afrika. Barabara za Zakongwe zilikuwa zimeharibika. Miti ilikuwa imekatwa na dhiki kuu za *Umero-Japa* kuathiri maisha ya wenyeji. Japo kulikuwa na mashimo mengi ya madini, nyumba nyingi zilikuwa hazijakamilika. *Umero-Japa* ni jina linalosimamia walio na nguvu na uwezo kama vile mkoloni aliyewatumia Waafrika kujitajirisha. Mwingilianomatini unatumika hapa kuelezea hali hii ya ukata kwa kunukuu mazungumzo ya msafiri na sauti inayomweleza. Hii si dayalojia ya kawaida kwani nukuu yake inatolewa ndani ya aya kwa mfano;

"Nilipofika tu alipokuwa amesimama, niligotwa kipajini na kuambiwa, 'Simama hapa, hupiti bila kuyajua haya. Nilitii. Unayaona yale majengo? Niliulizwa. Yalikuwa yale yaliyojengwa nusu. Ehh nayaona, kwa nini hayajamalizwa? Niliuliza. Kimya. Wanaume wote wenye nguvu walisombwa na kuchukuliwa, nilielezwa" (uk 28).

Mkoloni alisababisha hali ya umaskini katika bara la Afrika kwa kuwachukua wanaume kwenda kupigana Vita Vya Dunia ambavyo hawakuvianzisha. Ni bayana hapa kuwa hali ya migogoro na vita katika jamii nyingi husababisha hali ya umaskini miongoni mwa raia kwa kvunja mshikamano wa familia mna miji.

Kabla ya kuja kwa wakoloni, Afrika ilikuwa na mfumo wake wa kuzalisha chakula kwa kila mtu na ukarimu wao ulionekana hata kwa namna walivyomkaribisha mkoloni mwenyewe. Hali ya umaskini ya kuwa na mapato kidogo waliweza kuimudu kwa kugawa chochote kidogo walichokuwa nacho. Hali hii imeelezwa kwa kutumia nukuu ya hadithi ya bibilia;

“Kabla sijasema lolote, mmoja wao alinitangulia na kusema; ‘Hata nanyi karibu tule. Chakula ni hiki tu tulicho nacho lakini hatutawanyima.’ Nikakumbuka kile kisa cha yule mwanamke wa Bibilia...”(uk 28).

Msimulizi ambaye hapa anaeleza akiwa kama mkoloni anazuru maeneo ya pangoni ambapo anagundua ya kwamba wenyeji hawa hawakuwa na hitaji muhimu kabisa la msingi yaani chakula hata ingawa alistaajabia ukarimu wao. Kisa hiki kilimkumbusha ile hadithi ya mwanamke wa bibilia aliyemkaribisha mtume wa Mungu kukila chakula cha mwisho alichokuwa amekibakisha. Haya ni matumizi mazuri ya MM kwa wale wanaoelewa hadithi hii ya *Elijah* kwa bibilia na inaangazia hali ya ulitima aliyokumbana nayo msimulizi.

Msimulizi anaendelea na safari yake ya kutafuta suluhu kwa matatizo ya kijiji chake. Aliweza kugundua kuwa umaskini pia ni tatizo linalokumba jamii nyingi ulimwenguni. Msimulizi anapokaribia mji wa Hiro, yaani Japan, anapatana na mzee anayemwelezea hali ya wenyeji wanaong’ang’ana kuondoa umaskini. Wao wanajihusisha na uundaji wa magari kuukuu ili kuwauzia vijiji vya maeneo ya chini. Wanafuata hivi kwa kuongozwa na mawazo ya *‘Heike Monogotari*’(uk 47), mwenyeji aliyekuwa na kiburi na ubinafsi. Maudhui haya yanajengwa kimwingilianomatini kwa vile mwandishi unampa mzee nafasi ya kuwa na dayalojia na Msafiri kabla ya kutoweka ghafla. Kabla ya dayalojia hii, Msimulizi anaokota karatasi inayonukuliwa moja kwa moja. Maelezo yake yanachangia kuonyesha jinsi watu wa Mwainu waliungana kuuondoa umaskini. Sehemu ya nukuu inasema:

“Uhusiano kati ya binadamu na Uasili au mazingira unapaswa kuwa wa kimapatano. Lazima tukumbuke kuwa watu wa visiwa hivi waliumbwa kuwa watu maalum na wana uwezo mkubwa wa kuiongoza dunia” (uk 46).

Watu hawa wamejua kuyamudu mazingira yao ili kuondoa janga la umaskini. Utendaji kazi pekee huweza kuondoa umaskini na kuwapa watu uwezo wa kichumi. Wenyeji hawa walifanya kazi zao kwa bidii ili kujikimu kimaisha na mwandishi anadokeza jambo hili ili liweze kuigwa na Waafrika.

Mbali na kufanya uvumbuzi huu wa faida za utendajikazi, Msimulizi anagundua pia kuwa nchi zilizoendelea zinaongeza hali ya umaskini katika nchi zinazoendelea. Nchi hizi zinawapa Waafrika mikopo na kuwalazimisha kulipa kwa riba ya juu ama wasipoweza kulipa madeni, rasilmali zao zinachukuliwa na nchi hizi. Nchi ya Marekani inayorejelewa kama P.P. inachezea Waafrika ilhali wao wana uwezo mkubwa kiuchumi. Hali hii inafafanuliwa vyema kupitia hadithi ya *Goliath* anayepiga *Daudi* (uk 70) alipomrushia jiwe kichwani kwa kumbwewe. Hii hadithi imeelezwa kinyume na anavyojua msimulizi kutoka kwa Bibilia ambapo Daudi ndiye aliyempiga Goliath. Uwezo wa Waafrika ni mdogo kama Daudi alivyokuwa mdogo kwa kimo. Anapigwa kichwa na Goliath ambaye ni jitu kubwa lenye uwezo mkubwa sana kiuchumi.

Nchi hizi zilizoendelea huwapa mikopo Waafrika lakini haziwasaidii kuondoa hali ya umaskini kwa sababu fedha hizi huishia kwa mikono ya viongozi wachache wenye tamaa. Maisha ya jamii nyingi huwapa wenye uwezo matunda mazuri ya kiuchumi. Umati mkubwa wa wasiojiweza hung’ang’ania masalio ya wenye uwezo. Msimulizi alipofika *Bustani ya Eden* ya II, aliona kiongozi kwenye paa la nyumba akiyala matunda aliyotunda kwenye mti na kuwatupia waliokuwa chini karibu na ngazi. Wao nao waliyala waliyopenda na wasiyo yataka waliyatupia umati mkubwa uliokuwa huko chini. Nukuu ya moja kwa moja inasema:

“Kila kiongozi anakaa huko juu paani, huko ndiko anakochumia matunda kwa urahisi na kuwatupia

watu walioko chini ambao ndio waliomshikia ngazi ya kupanda juu” (uk 69).

‘Edeni’ ya kwanza inayarejelewa hapa ni shamba linalopatikana katika hadithi ya Bibilia kitabu cha Mwanzo ambapo matunda mengi yalinawiri. Edeni hii ya pili inaporejelewa inaleta taswira ya shamba hilo la kila aina ya matunda. Igawa lilikuwa na matunda mengi kiongozi aliamua kutoka juu kuhusu yule ambaye angefaidi kule chini. Jazanda hii inasimamia nchi zilizoendelea na zinavyoendelea kuwanyanyasa maskini wa nchi zinazoendelea. Wanapotoa mikopo kwa viongozi inabainika kuwa viongozi hawa hujifaidi kwanza na kuwapa raia wa nchi zao masalio ya mikopo hii.

Mwandishi anayajenga haya maudhui ya umaskini Ki-MM kwa kusimulia kisa cha mkombozi aliyekimbilia nyumba nyingine kuepuka mateso kwao. Hapa anarejelea tena bara la Afrika ambapo shida ya umaskini inazua migogoro juu ya ugavi wa rasilmali. Msimulizi anasema:

‘Matatizo ya nyumba zote kijijini yafanana sana.’ Dhiki na matatizo yalifanana katika nyumba zote, kwani mtoto aligongwa na akina mama wazima walipokuwa wakikimbilia usalama, baada ya nyumba yao kuchomwa hawakuwa na makazi wala chakula (uk 74).

Utegemezi wa mikopo na misaada kutoka nchi zingine zimesambaratisha uchumi na kuendeleza umaskini katika nchi za Kiafrika. Mwandishi ananukuu kumbukizi za msimulizi Ki-MM kuhusu swala hili. Dondoo linasema:

“Nilikumbuka kisa kilichotokea siku fulani katika nchi yangu. Kuna wakati serikali ilipofuja pesa kununua magari mengi ajabu kwa kuwa kulikuwa na mkutano fulani wa viongozi wa nchi huru barani” (uk 111).

Kisa hiki kinaakisi kile kilichotendeka nchini Kenya mnamo mwaka wa 1988 ambapo pesa nyingi mno zilitumiwa kupamba sherehe za kuadhimisha miaka kumi ya mfumo wa Nyayo. Ufujaji huu wa pesa za mikopo unaendeleza hali ya umaskini kwani wachache tu miongoni mwa viongozi wa nchi hujipatia manufaa kibinafsi. Watawaliwa wengine wote wanabaki katika hali ya ukata.

Mwandishi anajadili swala hili la umaskini kwa kutumia mbinu hii ya MM katika sehemu nyingi hadithini. Kwa maoni yake, umaskini si jambo linalowaathiri Waafrika pekee ulimwenguni. Kuna nchi zingine zinazoathiriwa na hali hii. Kwa mfano anaposema:

“Niliyaangalia majengo hayo pamoja na jamaa wawili, watatu waliotokea hapa na pale. ‘kumbe hata huku wana matatizo?’ Niliyakumbuka maneno ya mwalimu wangu chuoni. ‘Msidhani mataifa ya kimagharibi ni pepo. Kuna maskini kupindukia, nikuwa tu hatuna njia za kuhakikisha” (uk 144).

MM inadhihirika pale ambapo maneno ya mwalimu yananukuliwa moja kwa moja kupitia kwa kumbukumbu za msimulizi. Mwalimu alikuwa anazungumzia suala ibuka la umaskini ambao haujui mipaka wala tabaka. Kufuatia maoni ya kijana mwelekezi wa msimulizi, hali ya umaskini inaendelea kuwakabili Waafrika, kwa sababu hawataki kufikiria njia za kujiboresha. Kijana huyu anasema:

“Tatizo lenu kuu, hamtaki kuukubali uhalisi wenu na kujitahidi kuubadilisha.... Niliyapitisha maneno yake akilini.... tatizo lenu kuu hamtaki kuukubali uhalisi wenu, na kujitahidi kuubadilisha. Unawaona ndugu zako hao....” Yaelekea ilikuwa kweli. (uk 113).

Mwandishi anatumia mbinu ya MM kwa kuyanukuu ili kuyakariri na kuyaradidi mawazo ya msimulizi kuhusu hali ya umaskini barani. Anaendelea Ki-MM kurejelea kisa alichokumbuka msimulizi kuhusu vijana wa kwao waliotorokea nchi zingine na baadaye kuchoma pasipoti zao ili wahitimu kuwa wakimbizi wa kisiasa.

Muungano wa watu katika jamii huweza kuondoa umaskini kama anavyodokezwa mwandishi kupitia kwa kifungu hiki. Viongozi wasijilimbikizie mali huku wakiwaacha wanaowatawala wakiselelea katika lindi la umaskini. Iwapo watayamudu mazingira yao kwa njia bora basi wataweza kuyatosheleza mahitaji yao na kuishi maisha yanayoridhisha watu wote katika jamii. Mwandishi ametumia nukuu , marejeleo na misimu kufafanulia hali hii ya umaskini.

## HITIMISHO

Kazi hii imechunguza vipengele vya mwingilianomatini na namna mwandishi alivyoutumia kujenga maudhui ya umaskini katika riwaya za *Musaleo!* na *Bina-Adamu!* Mawazo ya Kristeva katika nadharia ya MM ni kuwa fasihi hutokana na kuwepo kwa fasihi nyingine ulimwenguni. Mbinu hii ya MM imeonyesha namna ambavyo hali ya ulitima ulilemaza Afrika hadi sasa.

Mwandishi amejenga haya maudhui ya ulitima kwa njia mbalimbali ikiwemo kutumia MM ili kuonyesha katika hadithi hizi hali ilivyokuwa awali na sasa barani Afrika.

Imebainika kuwa licha ya sera na uongozi mbaya ulioletwa na mkoloni, tatizo hili la umaskini limechangiwa na tabia za viongozi wabadhirifu na wasiowajibika. Wao wameendelea kudidimiza Waafrika katika lindi la ulitima hata baada ya nchi nyingi kujipatia uhuru na kumtimua mkoloni.

Suluhu kwa tatizo hili ni kuwahimiza wenyeji wa nchi hizi kuungana pamoja katika utendaji kazi na kurudia tena yale maadili asilia ya Kiafrika. Waafrika wanahitaji kubadili mienendo yao ili kuzuia hali ya umaskini kukita mizizi miongoni mwa jamii nyingi.

Fasihi za maeneo tofauti, nukuu na yale marejeleo anazotoa mwandishi zimetumiwa kuyajenga maudhui haya mbali na Istilahi zilizotumika zinazopatikana katika jamii za dunia.

## MAREJELEO

Hebel, U. J. (1989). Intertextuality, allusion, and quotation: an international bibliography of critical studies (Vol. 18). Greenwood Pub Group.

Olali,T. (2003) *Signs of New Features in the Swahili Novel*. Babu Alipofufuka na Watu wa Gehena http://www.qucosa.de/.../ 12-03-Diegner.pdf.

Selden, R.,Widdowson, P., & Booker, P. (2005): *A Readers Guide To LiteraryTheory*. 5th Ed. Great Britain. Pearson Longman.

Simmons, F.J. (2013).*Romantic and Contemporary Poetry:* http://www moodle.c.qu.edu.au

Herms, I. TUKI 2004. Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la Pili.[A standard Swahili dictionary. ]. Nairobi: Oxford University Press. xviii, 477 pp. ISBN 0195732227.

Wamitila, K. W. (2005).*Musaleo!* Nairobi. Vide-Muwa.

Wamitila, K.W. (2003).*Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Limited